PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji 2006/2025 ilianza kutekelezwa mwaka 2006. Programu hii inatekelezwa nchi nzima (Tanzania Bara)

Madhumuni ya Programu ni:kutekeleza Sera ya Maji, kama ilivyofafanuliwa katika Mkakati wa Maendeleo wa Sekta ya Maji inatekeleza mipango inayolenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji, kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira na kutekeleza mipango kwa njia ya uwiano wa sekta nzima.

Programu ina programu ndogo nne ambazo ni:- Usimamizi wa Raslimali za Maji Uendelezaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Uendelezaji wa Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini, na Uimarishaji wa mfumo wa kitaasisi na kuzijengea uwezo.

PROGRAMU NDOGO NNE ZA WSDP

1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Malengo makuu ni:

- Kuandaa mpango bora wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde tisa ya Maji hapa nchini.

- Kuimarisha matumizi bora ya rasilimali za maji ambapo usimamizi wa rasilimali za maji hufanywa na watumiaji wenyewe; utoaji wa maamuzi kufanyika kwa njia shirikishi na ya wazi, na kuweka uwajibikaji na umiliki wa hati ya matumizi ya maji kwa watumiaji wenyewe, ikiwa ni pamoja na makundi mbalimbali ya jamii, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Bodi za Mabonde ya Maji.

- Kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji ili ziweze kusimamia vizuri zaidi masuala ya rasilimali za maji zinazomilikiwa na Tanzania pamoja na zile tunazochangia na nchi nyingine.

Malengo mahsusi ni:

- Kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji kwa kuongeza watumishi na kuwapa mafunzo, ofisi na vitendeakazi

- Kuhusisha masuala ya sera, sheria na mabadiliko yaliyopo katika sekta zingine zinazohusiana na maji na yale ya rasilimali za maji.

- Kusajili na kutoa leseni kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya maji, ikiwa ni pamoja na uzuiaji wa uchafuzi wa rasilimali za maji, kulingana na Sera ya Maji. Hii pia pamoja na kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa kisheria.

- Kuandaa na kusimamia mpango wa kudhibiti ubora na uchafuzi wa mazingira ya vyanzo vya maji, na kuhakikisha viwango vya kudumu vya ubora wa maji, na utumiaji wa rasilimali za maji vinafuatwa.

- Kufanya tathmini ya rasilimali za maji hapa nchini na.
- Kujenga na kuzimarisha maabara za maji.

Vipengele katika Programu ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji

- Mpango wa Kitaifa wa uboreshaji na uwekezaji
- Mpango wa Kimabonde wa uboreshaji na uwekezaji
- Mpango wa Kitaifa wa uwekezaji katika masuala ya kisekta kwa jumla.

Utaratibu wa usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Usimamizi uko katika ngazi mbalimbali za kitaifa, mabonde na mabonde madogo.

Ngazi ya Taifa

- Wizara ya Maji inasimamia utekelezaji wa masuala ya kitaifa na yale yanayohusisha zaidi ya sekta moja kwa kushirikiana na taasisi nyingine.
- Kuandaa miongozo kwa ajili ya matumizi ya wadau mbalimbali
- Kutoa ushauri kwenye ngazi ya mabonde
- Kuandaa mpango wa mwaka wa programu ndogo ya usimamizi wa rasilimali za maji kupitia bodi ya ushauri .
- Bodi ya ushauri kumshauri Waziri wa Maji na kupitia masuala mbalimbali ya maji, ikiwa ni pamoja na masuala ya rufaa kuhusu matumizi ya maji.

Ngazi ya Mabonde

- Bodi za mabonde ya maji zina jukumu la kusimamia utendaji wa kila siku wa Ofisi za Mabonde ya Maji.

- Yana kazi ya hupitisha mipango na bajeti za Ofisi za Mabonde ya Maji kabla ya kuwasilishwa Wizarani kuona kama Sera na miongozo iliyowekwa inafuatwa.

- Watekelezaji katika ngazi ya bonde ni Ofisi za Mabonde ya Maji, ambazo ndizo zina wataalamu mbalimbali wanaotekeleza kazi zilizopo na maelekezo yanayotolewa na Bodi.

Ngazi ya Mabonde Madogo

- Katika mabonde madogo utaratibu umewekwa kwa ajili ya kusimamia masuala yaliyopo katika mabonde hayo, kabla ya kufikishwa kwenye ngazi ya Bonde.

Ngazi ya Jamii

- Jamii ndiyo inayounda vyombo vya watumiaji maji, mfano vikundi vya umwagiliaji, lengo ni kuimarisha na kudumisha matumizi bora ya maji.

Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Japokuwa mipaka ya mabonde ya maji haifuati mipaka ya kiutawala ya Mikoa wala Wilaya, Ofisi za Mabonde zinafanya kazi ndani ya maeneo hayo ambayo ndiyo yenye wananchi.

- Ofisi za Mabonde zitafanya kazi zinazohusu wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri husika kupitia Kamati za Maji na Usafi wa Mazingira ya Wilaya ambazo zimeanzishwa katika kila wilaya.

Miongozo ya Utekelezaji

Wizara ya Maji imeandaa miongozo na kusambazwa kwenye Ofisi za Mabonde yote Tisa ya Maji kwa ajili ya utekelezaji. Hadi sasa kuna miongozo miwili imekwisha andaliwa na kusambazwa kwa wananchi.

Masuala ya Fedha
Maandalizi ya Bajeti

Bajeti kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji zitaandaliwa kupitia ngazi husika. Bajeti hizo zitajadiliwa kwenye ngazi ya Bodi za Mabonde na Wizara na hatimaye kwenye Bodi ya Ushauri ya Kitaifa kwa ajili ya kuidhinishwa.

2. Programu Ndogo ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

Lengo kuu la programu

- Lengo kuu ni uboreshaji wa huduma ya maji ya kunywa na kuhakikisha yanapatikana kwa wingi na kwa ubora unafaa pamoja na usafi wa mazingira vijijini.

Lengo mahsusi ni:

- kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira endelevu vijijini na kwa uwiano mzuri kwa kuongeza huduma hiyo kutoka 55.7% (2006) hadi 65% mwaka (2010), 74% (2015) na 90% (2025).

Vipengele katika programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

- Kuimarisha, kujenga uwezo na kuweka mfumo wa kitaasisi na majukumu ya wadau kwa ajili ya watekelezaji katika ngazi mbalimbali.
- Kuzijengea uwezo Halmashauri zote hapa nchini ili ziweze kutekeleza majukumu yake vizuri.
- Kuboresha usafi wa mazingira.

Majukumu ya Wadau:

Ngazi ya Kitaifa

- Kuandaa miongozo ya utekelezaji na
- Kuratibu utekelezaji wa programu.

Ngazi ya Mkoa

- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Halmashauri zote na
- Ni kiungo kati ya Wizara na Halmashauri.

Ngazi ya Halmashauri

- Kutekeleza miradi,
- Kusaidia jamii kutambua mahitaji yao yanayohusiana na maji,
- Kutoa ushauri wa kifundi na kifedha kwa jamii na
- Kuwa kiungo kati ya mkoa na wananchi.

Ngazi ya Jamii

- Kuibua miradi ya maji,
- Kutekeleza miradi midogo na
- Kusimamia na kuendesha miradi kwa kuunda vyombo vya watumiaji maji na kuvisajili ili visimamie undeshaji wa miradi kisheria.

Sekta Binafsi

- Zitatekeleza miradi kupitia njia ya zabuni; kazi hizo ni pamoja na
- Kusaidia jamii kubuni, kupanga, kusanifu na kujenga miradi.

Kuimarisha Uwezo wa Halmashauri

- Kujenga au kukarabati ofisi za Idara ya Maji
- Kununua magari kwa ajili ya kila Halmashauri
- Kununua vitendeakazi ikiwa ni pamoja na kompyuta.

Ujenzi wa Miradi ya Maji

Utafiti uliofanyika mwaka 2003 katika wilaya 18, ulibaini kuwa katika kutekeleza programu kutakuwa na aina mbalimbali ya miraditakayojengwa hapa nchini kama ifuatavyo:

- Visima vifupi vya pampu za mkono, 31%
- Visima virefu vya pampu za mkono na 17%
- Miradi mchanganyiko ya bomba + mashine ya kusukuma maji 13%
- Mradi mmoja wa bomba + mashine ya kusukuma maji 12%
- Maji ya bomba ya mtiririko - vijiji vingi 12%
- Maji ya bomba ya mtiririko - kijiji kimoja 8%
- Mabwawa madogo 2%
- Uvunaji wa maji ya mvua 3%
- Mashine ya upepo 1%

- Kuboresha visima vya asili 1%

Usafi wa Mazingira

- Elimu itatolewa kuhusu usafi wa mazingira
- Vikundi vitaundwa kwenye shule za msingi na vijijini kwa lengo la kuwa kitovu cha uhamasishaji katika maeneo ya vijijini.

- Mafundi binafsi watapewa mafunzo kuhusu ujenzi wa vyoo bora ili kuweza kutoa huduma kwa jamii.

Wataalamu Washauri katika ngazi ya Halmashauri

Halmashauri zitaajiri wataalamu washauri kwa ajili ya:-

- Kuhamasisha jamii kuhusu utekelezaji wa WSDP katika maeneo yao
- Kupima na kusanifu miradi
- Kusimamia ujenzi wa miradi.

Wakandarasi katika ngazi ya Halmashauri

- Halmashauri zitaajiri wakandarasi kwa ajili ya kujenga miradi ya maji kwa niaba yao.

Miongozo ya utekelezaji

- Wizara ya Maji imeandaa miongozo na kuisambaza kwenye Halmashauri zote nchini kwa ajili ya matumizi katika utekelezaji.

- Hadi sasa, miongozo 15 imeandaliwa na kusambazwa kwa utekelezaji.

3. Programu Ndogo ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini

Lengo kuu la programu ni:

- kuboresha na kudumisha huduma ya majisafi na salama katika wingi na ubora unaofaa na utoaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka kwa maeneo ya mjini. Kwa kutumia Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini ambazo zinajitegemea kifedha na kufanya kazi kibiashara na kutoa huduma bora kwa bei nafuu.

Lengo mahsusi ni:

- Kuweka bei sahihi ya maji,
- Kusimamia matumizi bora ya maji,
- Kuwa na uhusiano mzuri na wateja na
- Kudhibiti uvujaji wa maji na kuongeza utoaji wa huduma ya majisafi kama ifuatavyo:-

i. Majisafi kutoka 78% (2006) hadi 90% (2010), 95% (2015) na 100% (2025)
ii. Uondoaji wa majitaka kutoka 17% (2006) hadi 30% (2010)

Vipengele katika programu hii ni:

- Kuimarisha uendeshaji kwenye mamlaka za Majisafi na Majitaka na
- Uwekezaji katika miradi ya maji vijijini.

Uwekezaji

Uwekezaji unahusisha mamlaka zote za ngazi za mkoa, Wilaya na Miji midogo ambapo;

- Miradi itabuniwa katika kila mji na utekelezaji utafanyika kwa kuchagua miji kufuatana na vigezo vilivyowekwa,
- Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo itaundiwa Mamlaka na kujengewa uwezo ili ijiendeshe kibiashara kama Miji Mikuu ya mkoa
- Miji Midogo ya Wilaya na Miji Mikuu ya Mikoa sasa inasimamiwa na **Idara ya Maji Kibiashara na siyo Idara ya Maji Kijamii.**

Kuimarisha uendeshaji kwenye mamlaka.

- Mamlaka zitarekebisha menejimenti na mifumo ya kitaasisi ili ziweze kujiendesha kibiashara.
- Kazi zingine zitafanywa na sekta binafsi ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi katika utendaji na tija.

Taratibu za utekelezaji

- Mamlaka (UWSAs) zitabadilishwa kuwa WSSAs
- WSSAs zitapewa leseni za kufanya biashara ya maji
- WSSAs zitasimamiwa na Bodi
- Kila WSSA itakuwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji Maji *(Consumers Consultative Council)* ambalo litakuwepo kwa niaba ya wananchi.

- Kwa utaratibu huo, masuala ya uendeshaji yatatekelezwa na menejimenti ikisimamiwa na Bodi, ambapo udhibiti utafanywa na chombo tofauti, EWURA. Maana yake ni kuwa kitu kimoja kinafanywa na chombo kimoja, badala ya vitu vyote kufanywa na chombo kimoja.

- EWURA kazi yake ni udhibiti kwa kufuata vigezo vya ufanisi (perfomance indicators), hususan vigezo vya kifedha (*financial)* na matokeo ya utoaji wa huduma ya maji, na siyo kwa kufuata mambo (*process*) yaliyofanikisha matokeo

Miongozo ya Utekelezaji

- Wizara imeandaa miongozo na kuisambaza kwenye mamlaka na EWURA, kwa ajili ya utekelezaji na

- Hadi sasa, miongozo miwili imeandaliwa na kusambazwa.

4. Programu Ndogo ya Kujenga Uwezo wa Taasisi

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ina kipengele cha kujenga uwezo wa taasisi zinazojihusisha na sekta ya maji ambapo:

- Uwezo utajengwa kwa kila ngazi na idara ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi hii ni pamoja na magari na kompyuta.

.

TARATIBU ZA HIFADHI YA JAMII NA MAZINGIRA

Katika kutekeleza WSDP, taratibu za hifadhi ya jamii na mazingira zimewekwa, kama ifuatavyo:

Environmental and Social Management Framework(kiswahili chake ...)
Utaratibu huu unaunganisha athari ya kijamii na mazingira, katika kutekeleza miradi.

Resettlement Policy Framework (kiswahili chake ...)

- Utaratibu huu unataka kuwa endapo jamii italazimika kuhama ili kutoa nafasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji, hapanabudi jamii hiyo ilipwe fidia kabla ya kuhama. Aidha, utaratibu huu unakataza kushurutisha jamii kuhama bila kulipwa fidia.

WAKALA

WSDP itajengea uwezo DDCA, Chuo cha Maji na Bohari Kuu ya Maji. Lengo la WSDP kuhusu Wakala ni kuziimarisha ili zishiriki kikamilifu katika programu, na ziweze kujiendesha kibiashara na kujitegemea kifedha ambapo.

- Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa inatakiwa ijitegemee kifedha ifikapo mwaka 2010.
- **Bohari Kuu la Maji:** lengo ni kuwa Wakala ijitegemee kifedha ifikapo mwaka 2010.
- **Chuo cha Maji**: lengo ni kuwa Wakala kujitegemee kifedha ifikapo mwaka 2015.
- Uimarishaji wa vyombo hivi utafanyika kwa kutoa vifaa vya kufanyia kazi, na watumishi.

EWURA

EWURA ni mamlaka iliyoundwa kisheria kwa ajili ya kudhibiti matumizi ya nishati na maji. Tayari chombo hiki kinafanya kazi zake.

- EWURA itafanya udhibiti katika utoaji wa huduma ya maji mijini,
- Kwa sasa ni baadhi ya mamlaka ndizo zinasimamiwa na EWURA.
- EWURA inatoa leseni kwa mamlaka kwa ajili ya kuendesha huduma ya maji kibiashara.

MAHITAJI YA FEDHA ZA WSDP KWA JUMLA

- Kati ya mwaka 2006 – 2010, jumla ya USD 951 milioni zinahitajika.
- Fedha hizo zitachangiwa kati ya Washirika wa Maendeleo na Serikali ya Tanzania
- Washirika wa Maendeleo watachangia kiasi cha USD 700 milioni
- Serikali itachangia kiasi cha USD 251 milioni.

USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA WSDP

- Chini ya WSDP, utaratibu umewekwa ili kufuatilia na utekelezaji wa programu
- Utaratibu wa aina ya kwanza ni kwa kupokea taarifa kutoka kwa watekelezaji, kuzichambua na kutoa ushauri.
- Utaratibu wa aina ya pili ni kwenda kukagua miradi na kutoa ushauri katika maeneo ya utekelezaji.
- Utaratibu wa aina ya tatu ni kwa kutumia mijadala ya wadau. Katika utaratibu huo, kamati ndogo mbalimbali zitakutana ili kujadili masuala ya aina moja. Taarifa za kamati hizo zitapelekwa kwenye kamati ya ngazi inayofuata (WSWG) kwa taarifa na uamuzi zaidi. Taarifa kutoka kwenye WSWG zitapelekwa kwenye Mkutano wa pamoja wa Wadau wa Mapitio ya Utekelezaji, ambao hukaa mara moja kwa mwaka.